**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 7, Issue 1, 2024**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Changamoto Zinazokumba Shirika la Utangazaji la Uganda Katika Kukikuza Kiswahili Jijini Kampala

*Monday Geofrey Akol[1*], Sheila Pamela Wandera-Simwa[1] na Onyango Ogola James[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Laikipia, S. L. P. 1100 – 20300 Nyahururu, Kenya.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: mwalimakol@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2200**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*09 Septemba 2024*

**Istilahi Muhimu**:

*Changamoto, Shirika la Utangazaji, Kukikuza Kiswahili, Kampala.*

## IKISIRI

Kiswahili nchini Uganda kimetumiwa tangu enzi za kabla ya ukoloni katika tasnia mbalimbali ila bado hakijaenea kama inavyostahili. Licha ya kuwa Uganda kuna sera, mazoea, na utaratibu wa kuendeleza Kiswahili, bado kina wakati mgumu kupenyeza kila mahali huku baadhi ya jamii ya Wanauganda wakibaki kuwa na mtazamo hasi kuhusu lugha hii adimu. Tafiti za awali zilionyesha kuwa mashirika ya utangazaji ya serikali ni muhimu sana katika kukuza lugha za mawasiliano ulimwenguni. Nchini Uganda, mtafiti hajakumbana na utafiti unaoonyesha chanagamoto zinazolikumba Shirika la Utangazaji la Uganda katika kukuza lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo utafiti huu ulinuia kutathmini changamoto zinazokumba Shirika la Utangazaji la Uganda katika kukikuza Kiswahili jijini Kampala. Utafiti ulitumia nadharia ya upangaji lugha kubaini hasa jinsi shirika hilo lenye vituo kumi na moja vya redio na vinne vya televisheni linavyokumbana na changamoto za kukuza Kiswahili katika jiji kuu la Kampala. Kwa kutumia nadharia hiyo utafiti uliegemea sana itikadi nne za upangaji lugha na vipengele vinne vya mchakato wa usanifishaji wa lugha hasa kile cha uimarishaji wa lugha. Mbinu za kurekodi, mahojiano, uchunzaji wa kushiriki na kusoma maktabani zilitumika katika kukusanya data. Sampuli ya utafiti huu kwa jumla ilihusisha watu 30 wakiwemo watumishi 20 wa Shirika la Utangazaji la Uganda ambapo 10 ni Waandishi Habari za Kiswahili. Watu 10 waliosalia waliteuliwa kutoka hadhira ya Shirika la Utangazaji la Uganda jijini Kampala. Utafiti huu uliwalenga wasikilizaji, watazamaji, watumishi wa makao makuu ya Shirika la Utangazaji Uganda jijini Kampala kwa vile wao ndio wadau waliochangia kwa kufanikisha madhumuni ya utafiti huu. Utafiti huu ulibainisha kuwa kuna wataalamu wachache katika lugha ya Kiswahili, ukosefu wa wahisani na ufadhili, kutokuwepo kwa sera madhubuti ya uhariri kuhusu Kiswahili, uhaba wa vitendea kazi na mitazamo hasi kwa lugha ya Kiswahili ni baadhi ya changamoto zinazokumba shirika la Utangazaji la Uganda katika harakati zake za kuendeleza lugha ya Kiswahili. Utafiti huu una manufaa kwa wizara zinazoshughulika na maendeleo ya Kiswahili Uganda kwa sababu vile utawapa mwanga kuhusu changamoto zinazolikumba Shirika la Utangazaji la Uganda katika harakati za kukukuza Kiswahili.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2200

**APA CITATION**

Akol, M. G., Wandera-Simwa, S. P. & Ogola, J. O. (2024). Changamoto Zinazokumba Shirika la Utangazaji la Uganda Katika Kukikuza Kiswahili Jijini Kampala. *East African Journal of Swahili Studies*, *7*(1), 395-404. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2200.

**CHICAGO CITATION**

Akol, Monday Geofrey, Sheila Pamela Wandera-Simwa and James Onyango Ogola. 2024. "Changamoto Zinazokumba Shirika la Utangazaji la Uganda Katika Kukikuza Kiswahili Jijini Kampala". *East African Journal of Swahili Studies* 7 (1), 395-404. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2200

**HARVARD CITATION**

Akol, M. G., Wandera-Simwa, S. P. & Ogola, J. O. (2024) "Changamoto Zinazokumba Shirika la Utangazaji la Uganda Katika Kukikuza Kiswahili Jijini Kampala", *East African Journal of Swahili Studies*, 7(1), pp. 395-404. doi: 10.37284/jammk.7.1.2200

**IEEE CITATION**

M. G. Akol, S. P. Wandera-Simwa & J. O. Ogola "Changamoto Zinazokumba Shirika la Utangazaji la Uganda Katika Kukikuza Kiswahili Jijini Kampala", *EAJSS*, vol. 7, no. 1, pp. 395-404, Sep. 2024.

**MLA CITATION**

Akol, Monday Geofrey, Sheila Pamela Wandera-Simwa & James Onyango Ogola. "Changamoto Zinazokumba Shirika la Utangazaji la Uganda Katika Kukikuza Kiswahili Jijini Kampala". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 7, no. 1, Sep. 2024, pp. 395-404, doi:10.37284/jammk.7.1.2200.

## UTANGULIZI

Kiswahili nchini Uganda kilikuwepo hata kabla ya ukoloni. Kilitumiwa sana katika biashara huku Waarabu kutoka pwani na mawakala wao wakikitumia kuendeleza shughuli zao kama za biashara ya watumwa. Uganda ilishiriki katika shughuli za kukikuza Kiswahili kabla ya ukoloni hadi mwaka 1964 ilipojitoa baada ya serikali ya Dkt. Milton Obote kupata upinzani mkali kutoka kwa jamii ya Waganda kuhusu lugha gani iwe lugha ya taifa kati ya Kiswahili na Kiluganda. Kutokuwepo na chombo rasmi cha kusimamia na kuratibu maendeleo ya Kiswahili kwa muda mrefu ni changamoto kwa ukuaji wa lugha ya Kiswahili ukijumuisha kwamba bado idadi ya wataalamu wa Kiswahili ni ndogo sana nchini Uganda. Vyombo vya habari ni muhimu sana katika ukuaji wa lugha ya Kiswahili nchini Uganda. Katika shirika la UBC Kiswahili kinatajwa tu kama lugha inayofaa kutumiwa katika shughuli za matangazo lakini hakijapewa hadhi yake kama lugha rasmi ya pili. Isitoshe muda uliotengwa kwa ajili ya Kiswahili ni mdogo ukilinganishwa na Kiingereza na Kiluganda.

Kwa hiyo ukosefu wa sera madhubuti ya uhariri kuhusu Kiswahili bado ni changamoto. Maendeleo na ukuzaji wa Kiswahili UBC mara nyingi hutegemea utawala. Utawala unapokuwa na watu wanaokipenda Kiswahili, vipindi na shughuli za Kiswahili zinaongezeka. Na utawala unapokuwa na watu wenye msimamo hasi kuhusu Kiswahili, shughuli za Kiswahili hupungua sana. Shirika la utangazaji la Uganda (UBC) ni mojawapo ya vyombo vya habari vinavyoendeleza lugha hii ya Kiswahili. Katika harakati za kuendeleza lugha ya Kiswahili miongoni mwa Wanauganda, shirika hili linakumbwa na changamoto nyingi sana. Kwa hivyo Makala hii inatarajiwa kutathmini changamoto zinazokumba Shirika la Utangazaji la Uganda (UBC) katika kukikuza Kiswahili jijini Kampala.

### Mapitio ya Maandishi

Ababakar (2013) alitafiti kuhusu changamoto zinazoikumba lugha ya Kiswahili ulimwenguni na kusema kuwa kuna changamoto nyingi ambazo zinakwamiza maendeleo ya lugha hii. Aligundua kuwa lugha ya Kiswahili inakosa vitabu vya kuwafundishia wageni lugha hii. Kulingana na Kinge'i (2000), uandishi wa habari ni uwanja maalum wa kimatumizi ambapo ubora wa makala za habari hutegemea ujuzi wa mtindo wa mwandishi husika. Ujuzi wa waandishi habari za Kiswahili si Uganda tu mara nyingi umetiliwa shaka na kusababisha shughuli nzima ya vyombo vya habari kukuza lugha hii muruwa kukwama.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2200

Miima na Kawoya (2021) wanasema kuwa Kiswahili ni lugha inayopitia changamoto nyingi nchini Uganda. Wanaendelea kueleza kuwa kuna uhaba wa maandishi na vitabu vya Kiswahili nchini Uganda. Vitabu na maandishi ya Kiswahili ambayo yanapatikana nchini Uganda yameandikwa na waandishi ambao si Wanauganda na kwa hivyo maandishi haya hayaashirii utamaduni wa Wanauganda. Nchini Uganda, maenezi ya Kiswahili yalitingwa na viongozi (Kiango, 2002). Anaeleza kuwa pendekezo la kuifanya lugha ya Kiswahili iwe lugha ya kufundishia shuleni, lugha ya utawala, na lugha ya mawasiliano nchini Uganda lilipingwa na viongozi wa jadi wa jamii ya Waganda ikiwa ni pamoja na Kabaka Sir Daudi Chwa mwaka 1929 pamoja na mrithi wake Kabaka Sir Edward Mutesa II miaka ya 1960 - 1965. Lugha ya Kiswahili ilitumiwa tu na wananchi ambao hawakujua lugha za Kiluganda na Kiingereza. Lugha hii ilitumiwa na polisi na sehemu za michezo tu. Ili kutinga maendelezi ya Kiswahili zaidi, lugha ya Kingereza iliteuliwa kama lugha rasmi kutumiwa katika shughuli za kitaifa na kimataifa .

## Nadharia ya Upangaji Lugha

Nadharia ya upangaji lugha iliasisiwa na msomi Einar Haugen ambaye aliendeleza dhana ya upangaji lugha katika utafiti wake wa jinsi viwango mbalimbali vya kisasa vya lugha ya Kinoruwe vilivyoundwa (Haugen,1959). Mwanzoni Haugen aliutambua upangaji lugha kama kuandaa sarufi ya kawaida, utunzi wa nukuu na kamusi kwa kuwaongoza waandishi na wasemaji katika jamii ya lugha na lahaja nyingi. Haugen (1959) aliendelea kuelezea kutoa mtazamo dhahania kuwa upangaji lugha ni tathmini ya mabadiliko ya isimu. Haugen (1966) alishauri kuwa utafiti katika upangaji lugha lazima uangazie mawakala na wadau wanaohusika katika mchakato wa upangaji lugha. Haugen (1959) anasema kuwa mchakato wa upangaji lugha una hatua au ngazi nne ikiwa ni pamoja na; kuchagua lugha kama chombo cha mawasiliano, kusanifisha, kuweka kanuni za lugha kama chombo cha mawasiliano au uimarishaji, utekelezaji wa matumizi yake na kuelezea matumizi.

Kwa kuongozwa na kazi yake Haugen (1983), utafiti huu uliangazia hatua za nadharia ya upangaji lugha katika utafiti huu. Hatua iliyotumiwa ni ile ya kuchagua lugha kama chombo cha mawasiliano. Katika hatua hii lazima malengo na mipaka ya lugha iliyochaguliwa yawekwe wazi. Shirika la Utangazaji la Uganda (UBC) kama shirika la utangazaji la taifa limechagua lugha za kutumia katika shughuli zake za utangazaji. Kiswahili ni mojawapo ya lugha hizo na utafiti huu uliweka mwanga juu ya changamoto za Shirika la Utangazaji la Uganda za kuchagua Kiswahili miongoni mwa lugha za kutumia katika shughuli zake.

## Mbinu za Utafiti

Utafiti huu ulitumia muundo wa kimaelezo kwa sababu data katika utafiti huu zilikuwa za kithamano. Utafiti ulifanyika jijini Kampala katika makao makuu ya Shirika la Utangazaji Uganda. Mji wa Kampala ulichaguliwa kama mahali pa utafiti kwa sababu ndio mji mkuu wa nchi ya Uganda. Mbinu za kurekodi, mahojiano, uchunzaji wa kushiriki na kusoma maktabani zilitumika katika kukusanya data. Sampuli ya utafiti huu kwa jumla ilihusisha watu 30 wakiwemo watumishi 20 wa Shirika la Utangazaji la Uganda ambapo 10 ni Waandishi Habari za Kiswahili. Watu 10 waliosalia waliteuliwa kutoka hadhira ya Shirika la Utangazaji la Uganda jijini Kampala. Utafiti huu uliwalenga wasikilizaji, watazamaji, watumishi wa makao makuu ya Shirika la Utangazaji Uganda jijini Kampala kwa vile wao ndio wadau waliochangia kwa kufanikisha madhumuni ya utafiti huu.Utafiti ulikilenga kikundi hiki cha watu kwa sababu ni hao ndio husikiliza na kutazama vipindi vya Shirika la Utangazaji Uganda.Utafiti huu ulitumia mbinu ya kimakusudi kuchagua sampuli ya utafiti. Utafiti ulitumia watumishi 20 wanaohusika na masuala ya utangazaji katika Shirika la Utangazaji la Uganda ambapo watumishi 10 walikuwa waandishi wa habari za Kiswahili. Data katika makala hii zilipatikana kutokana na mbinu za mahojiano, kusoma, na

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2200

maswali ya hojaji. Mbinu ya kimaelezo ilitumiwa katika uchanganuzi na uwasilishaji wa data.

## Matokeo ya Utafiti

### Mtazamo Hasi kwa Lugha ya Kiswahili

Mtazamo hasi miongoni mwa wakaazi wa jiji la Kampala kuhusu lugha ya Kiswahili ni kikwamizo kikuu kwa vituo vya Shirika la Utangazaji la Uganda kukuza lugha ya Kiswahili katika jiji hili. Hali hii ni sawa na maoni ya Bamgbose (1991)anayedai kuwa wazungumzaji wengi huzidunisha lugha za Kiafrika ukizilinganisha na lugha za kigeni za Wazungu. Katika jiji la Kampala, watafitiwa nane kutoka hadhira ya Shirika la Utangazaji la Uganda wanakiri kuwa hawatumii lugha ya Kiswahili kwa sababu ni lugha ambayo haina umuhimu wowote kwa maisha yao. Nane hao hufanya kazi katika ofisi ambapo na stakabadhi zote za kiserikali hutumia lugha ya Kiingereza kwa wingi. Katika hali hii, lugha ya Kiswahili huonekana kama lugha isiyotumiwa katika shughuli muhimu kama vile kuandaa makala muhimu serikalini na matumizi ya ofisini.

Wasikilizaji kumi wa Shirika la Utangazaji la Uganda walikiri kuwa lugha ya Kiswahili ni lugha ambayo inastahili kutumiwa na watu walio na kiwango cha chini cha elimu. Wakaazi mjini Kampala walio na elimu ya juu kama vile elimu ya vyuo vikuu hutumia lugha ya Kiingereza katika shughuli zao za kiofisi. Kiswahili ni lugha ambayo wakaazi wa mji mkuu wa Kampala huiona kama lugha duni kwa sababu hata bunge la Uganda halijaidhinisha matumizi yake katika miktadha rasmi. Hali hii inaonyesha kuwa wakaazi wa mji mkuu wa Kampala hawaionei fahari lugha ya Kiswahili kama lugha yenye asili yake katika maeneo ya Afrika Mashariki. Kwa sababu ya mitazamo hasi miongoni mwa wakaazi wa mji mkuu wa Kampala, wahojiwa hawa walikubali kuwa wao hawatazami vipindi vya kituo cha UBC vinavyotumia lugha ya Kiswahili. Pia, wahojiwa walikiri kuwa hawasikilizi vipindi vya redio katika kituo cha Shirika la Utangazaji la Uganda vinavyotoa matangazo katika lugha ya Kiswahili. Ilibainika katika mahojiano kuwa wakaaji wa mji mkuu wa Kampala hawanunui jarida la *Mwangaza* ambalo huandikwa katika lugha ya Kiswahili. Hali hii inafanya Shirika la Utangazaji la Uganda kuwa na wakati mgumu kuikuza lugha ya Kiswahili miongoni mwa wakaazi wa mji mkuu wa Kampala. Hii ni kwa sababu wakaazi hawa hawapati mafunzo ya Kiswahili kutoka Shirika la Utangazaji la Uganda. Wasipopata mwelekeo halisi katika lugha ya Kiswahili, hawatajua kutumia lugha ya Kiswahili ipasavyo. Wao wanaendelea kutumia lugha ya Kiswahili visivyo na kueneza matumizi haya mabaya kwa vizazi vijavyo. Mwelekeo huu hasi huambukizwa kwa watoto na wao pia kuendelea kutumia lugha ya Kiswahili vibaya. Kwa hivyo matumizi mabaya katika lugha ya Kiswahili kwa wakaazi wa mji mkuu wa Kampala ni jambo ambalo limeigwa kutoka vizazi vilivyopita.

### Mfumo wa Elimu Unaoegemea Lugha ya Kiingereza

Shirika la utangazaji la Uganda linakumbwa na changamoto la kukuza lugha ya kiswahili miongoni mwa wakaaji wa mji wa Kampala kwa sababu ya mfumo wa elimu nchini Uganda. Kulingana na Victor (2019), kukuza na kuendeleza Kiswahili kunahitaji ushirikiano wa asasi mbalimbali. Asasi hizo zimekuwa zikitoa wataalamu wanaoshiriki katika vipindi vya redio na televisheni au kuhojiwa katika makala za magazeti mbalimbali kwa ajili ya kutoa taarifa, mafunzo, na maarifa kuhusu lugha ya Kiswahili. Asasi hizo ni wadau muhimu wa vyombo vya habari katika kusukuma pamoja gurudumu la maendeleo ya Kiswahili. Kando na asasi alizotaja Victor (2019), mfumo wa elimu ni mbinu muhimu sana katika kuendeleza na kukuza lugha ya Kiswahili miongoni mwa wakaazi wa mji wa Kampala.

Lugha ya Kiswahili itakuwa lugha rasmi ya pili nchini Uganda na itatumiwa kama bunge litakavyoamua kulingana na katiba ya Jamhuri ya Uganda ya 1995 (Miima na Kawoya, 2021). Hadi sasa bunge la nchi ya Uganda halijaidhinisha lugha ya Kiswahili kuwa lugha rasmi nchini humo. Hii ndio hadhi ya lugha ya Kiswahili nchini Uganda. Katika elimu, lugha ya Kiingereza ndio

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2200

lugha inayotumika kama lugha ya kufundishia masomo mengine. Kulingana na wakaazi wa mji wa Kampala waliohojiwa, lugha ya Kiswahili hutumiwa tu kufundishia somo la Kiswahili pekee. Kwa hivyo wanafunzi huzungumza lugha ya Kiswahili katika vipindi vya Kiswahili tu. Vipindi vingine shuleni hutawaliwa na lugha ya Kiingereza. Kwa hivyo wanafunzi hawajui kurejelea dhana nyingi katika lugha ya Kiswahili. Ni vigumu wanafunzi wa shule za Kampala kueleza masomo mengine katika lugha ya Kiswahili. Mitihani ya masomo mengine isipokuwa somo la Kiswahili huandaliwa katika lugha ya Kiingereza. Kwa hivyo wanafunzi huwa na fursa katika somo la Kiswahili pekee kueleza mawazo yao katika lugha ya Kiswahili.

Uchaguzi wa lugha ya Kiswahili kuwa lugha rasmi ya pili kufuatia lugha ya Kiingereza bila kuifanya kuwa lugha ya kufundishia shuleni ni suala ambalo hukwamiza matokeo ya utekelezaji katika maendeleo ya lugha ya Kiswahili. Lugha inayotumika katika kufundisha katika mifumo yote ya elimu ni Kiingereza. Hali kama hii imesababisha ugumu kwa Shirika la Utangazaji la Uganda kuendeleza lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu mfumo ulioko wa elimu hauwapi wanafunzi fursa ya kujifunza masomo mengine katika lugha ya Kiswahili. Tafiti zote za kielimu huandikwa katika lugha ya Kiingereza isipokuwa zile zinazofanywa katika somo la Kiswahili. Hali hii husababisha uchache wa makala ambayo yameandikwa katika lugha ya Kiswahili. Watafiti katika lugha ya Kiswahili huwa na makala chache za kuendeleza tafiti zao katika lugha ya Kiswahili. Hali hii hupunguza marejeleo ya kuendeleza tafiti zingine katika lugha ya Kiswahili. Hali hii husababisha ugumu katika tafiti za Kiswahili mjini Kampala na kwa watafiti wengi wakiwemo wale kutoka Shirika la Utangazaji la Uganda. Watafiti wa lugha ya Kiswahili mjini Kampala hufa moyo kwa sababu ya kazi nyingi ya kutafsiri makala kutoka lugha ya Kiingereza hadi Kiswahili. Mhojiwa II alisema kuwa;

> *"Shule za msingi zinazopatikana mjini Kampala kama vile shule ya Sir Apollo Kaggwa na ile ya Mtakatifu Francis hutumia lugha ya Kiingereza kufundisha masomo yote isipokuwa somo la Kiswahili ambalo hufunzwa katika lugha ya Kiswahili. Wanafunzi hivyo basi huwa na muda mchache wa kuizungumza lugha ya Kiswahili. Lugha ya Kiswahili hivyo basi huwa kama lugha geni kwa wanafunzi hawa wa shule za msingi. Hali ni ile ile katika shule za upili hapa mjini Kampala …".*

Kwa sababu ya changamoto hizi wasomi katika mji mkuu wa Kampala hawana makala ya lugha ya Kiswahili ya kufanyia mazoezi katika lugha ya Kiswahili. Hali hii husababisha ukosefu wa maarifa kwa wasomi wa lugha ya Kiswahili ambao wengine ni watangazaji wa Shirika la Utangazaji la Uganda. Watangazaji hawa basi huwa na changamoto kutayarisha vipindi vya lugha ya Kiswahili. Wao hivyo basi hawatekelezi kazi yao ya uendelezaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa wakaazi wa mji wa Kampala ipasavyo. Mhojiwa alisema kuwa;

> *"Lugha ya Kiswahili kwangu ni kama lugha geni, sijakuwa na uzoevu wa kuitumia lugha hii tangu utotoni. Ni lugha ambayo nimejifunza tu shuleni. Hata hivyo, shuleni tulijifunza Kiswahili kwa kutumia Kiluganda katika darasa ya chekechea hadi madarasa ya chini katika shule ya msingi. Kwa hivyo hata kama mtangazaji nina changamoto katika matumizi ya lugha ya Kiswahili …"*

**Athari Kutoka kwa Watangazaji**

Kulingana na Ryanga na Ngowa (2018) vyombo vya habari huweza kuwa na athari katika lugha. Wanaendelea kueleza kuwa athari zinapokuwa chanya huweza kuchangia katika ukuaji wa lugha hii na kuendelea kwake. Kwa upande mwingine athari zinaweza kuwa hasi na kuchangia uharibifu wa lugha. Athari za vyombo vya habari katika lugha ya Kiswahili pia zinaweza kutinga fonolojia, mofolojia, sintaksia na hata leksikolojia.

Watangazaji wa UBC hukwamiza maendeleo ya lugha ya Kiswahili kwa njia mbalimbali. Kwa upande wa matamshi, kuna watangazaji hutamka

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2200

maneno ya Kiswahili kwa njia isivyofaa. Watangazaji wa habari hutangaza kwa kutumia lugha isiyo sahihi. Waandishi wa habari pia huandika magazeti yaliyo na makosa katika lugha. Wanahabari wengine hutumia sentensi zenye makosa hadharani. Wengine hutumia misamiati pasipofaa na kwa njia inayopotosha. Kwa kufanya hivi, wanahabari hawa hutoa mwelekeo mbaya kwa wakaaji wa mji wa Kampala. Wengi wa wakaazi wa Kampala huiga mataumizi ya lugha ya Kiswahili jinsi inavyotumiwa katika Shirika la Utangazaji la UBC. Kuna mtangazaji mmoja ambaye hutoa buradani za futuhi alisikika akisema: *"*Ng'ombe yote iliibwa na wezi kutoka jamii jirani."*

> *Kuna yule aliyesema, *"mpango wenye ulipangwa umekamilika."*

Baada ya kusoma maandishi ya jarida la *Mwangaza a*mbalo huandikwa na waandishi wa Shirika la Utangazaji Uganda, kunaonesha waziwazi kuwa waandishi hawa wa habari hufanya makosa mbalimbali ya lugha kama vile yale ya kisarufi, makosa ya kiisimu ya utamkaji na semantiki. Utafiti huu uligundua kwamba miongoni mwa makosa yanayofanywa katika utoaji wa habari kwenye Shirika la Utangazaji la Uganda ni yale ya urudiaji maneno yasiyofaa kurudiwa, ukosefu wa ushikamano katika sentensi, makosa ya tahajia na makosa katika uchapaji wa maneno. Makosa ya kisarufi katika gazeti la Mwangaza na habari za watangazaji wa Shirika la Utangzaji la Uganda ni kero kwa wasomaji na watazamaji wa runinga na pia hushusha hadhi ya kituo cha Utangazaji cha Uganda. Makosa yanayofanywa na watangazaji na waandishi wa habari yanasababishwa na jamii, ukosefu wa weledi katika lugha ya Kiswahili na udhaifu wa binafsi wa wanahabari wenyewe. Wanafunzi katika vyuo vya uandishi wa habari na waandishi wa habari waliofuzu hawana ujuzi wa sarufi. Hali hii hutokea kwa sababu ya ufundishaji usiofaa wa sarufi katika vyuo vya wanahabari nchini Uganda.

Vichwa vya habari katika jarida la Mwangaza husheheni makosa kwa huvunja kanuni za kisarufi jambo ambalo hufanya habari kuwa ngumu kufasirika. Matangazo ya habari na magazeti katika Shirika la Utangazaji la Uganda husheheni matumzi mengi ya maneno ya mkopo kutoka lugha ya Kiingereza. Maneno haya hutumia miundo ya lugha ya Kiingereza na msamiati usio sanifu. Wakati mwingine kuna maneno ya mtaani. Wanahabari hufanya hivi kuwavutia wasomaji wa rika fulani bila kujua wanaua lugha ya Kiswahili katika mji wa Kampala. Katika kufanya makosa haya katika lugha ya Kiswahili na wanahabari katika Shirika la Utangazaji la Uganda, wanahabari hawa hupotosha wakaaji wa mji wa Kampala katika matumizi yao ya lugha. Wakaaji wengi wa mji wa Kampala hujifunza mengi kutokana na vipindi vya lugha ya Kiswahili yakiwemo haya makosa kwa sababu wao huchukulia kuwa kile kinachotangazwa katika runinga, televisheni au wanachosikia kwenye redio ni kweli. Kwa hivyo hali hii huwa vigumu sana kwa wananchi kujifunza lugha ya Kiswahili kupitia matangazo na vipindi vya shirika la Utangazaji la Uganda.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

East African Journal of Swahili Studies, Volume 7, Issue 1, 2024
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2200



KUSHEREHEKEA MIAKA 25 YA MAFANIKIO MUHIMU YA WANAWAKE UGANDA

Mhe. Frank Tumwebaze Waziri wa Jinsia, Ajira na Maendeleo ya Kijamii

Utanguliz

Siku kuu ya wanawake ya kimataifa inasherehekewa tarehe nane machi kila mwaka. Ni siku ya kimataifa inayojumuisha mafanikio ya utimizaji wa usawa wa kijinsia na uwezo kwa wanawake. Siku hii pia inaangazia kutoa wito kwa kuzidisha maendeleo juu ya usawa wa kijinsia na uwezo kwa wanawake.

Mwaka huu, 2020, siku kuu ya kimataifa ya wanawake itasherekewa juu ya kauli mbiu ya kimataifa ya, "Dunia yenye usawa ni dunia yenye uwezo" kauli mbiu hii inalenga na kujikita kwenye jukumu la taifa na watu binafsi kuchagua kwa dhati kushindisha kila aina yoyote ile ya ubaguzi, madharau, tashwishi, kupanua misimamo, kusherehekea mafanikio ya wanawake kwa pamoja na kujitolea kuchukua hatua dhamirifu ili kuzidisha mabadiliko chanya kwa suala la usawa wa kijinsia na uwezo kwa wanawake.

Na Mhe. Peace R. Mutuuzo Waziri wa Nchi wa Jinsia na Utamaduni, Mbuge wa Bunyangabo

Kauli mbiu iliyoteuliwa kwa sherehe za kitaifa ni, "Kusherehekea Miaka 25 Ya Katiba Ya Uganda Ya 1995: Mafanikio Muhimu Katika Ukuzaji Wa Usawa Wa Kijinsia Na Uwezo Kwa Wanawake Nchini Uganda". Mwaka 2020 unatoa hesabu kamili ya miaka 25 tangu katiba ya uganda ya 1995 ilivyoundwa na kuanza kutumika ikiwa ni pamoja na miaka 10 ya utekelezwaji wa mipango ya maendeleo ya kitaifa(NDP). Katiba ya 1995 ya jamahuri ya Uganda pamoja na vipengele vyake vinavyozingatia masuala ya kijinsia, imeelekeza ajenda ya kitaifa juu ya haki za wanawake. Uganda imepiga hatua katika kuweka na kungiza kanuni na mahitaji ya kimataifa na kikanda ya kufuatilia haki za wanawake ili kuwezesha utekelezwaji wake katika sekta zote. Ijapokuwa kuna ufanisi

7

Badala ya kufunza, shirika hili kwa wakati mwingine hupotosha.

> *Neno utangulizi limeandikwa visivyo katika makala haya.*

Watangazaji hawa husahau kuwa wao ni kioo cha jamii na kuna mambo mengi ambayo jamii hujifunza kutoka kwao. Wakaazi wa mji wa Kampala huiga lugha yenye makosa kutoka kwa watangazaji wa Shirika la Utangazaji la Uganda.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2200

Makosa mengine yanayotokea katika utangazaji huwa ya kimzaha lakini wasikilizaji huchukulia kuwa hivyo ndivyo inavyostahili kutumiwa. Wao hivyo basi huiga lugha yenye makosa kutoka kwa watangazaji na waandishi wa habari. Wanahabari hawa wamechukulia lugha ya Kiswahili kama lugha ya mizaha na hakuna aibu yoyote kwa yule anayevunja sheria za matumizi ya lugha ya Kiswahili. Hii ni kinyume na lugha ya Kiingereza ambapo yeyote anayevunja sheria za matumizi ya lugha ya Kiingereza hulazimika kuomba radhi na kufanya marekebisho papo hapo. Huu ni kama mwiba wa kujidunga, kwani shirika hili limezua mbinu mbalimbali za kuinua kiwango cha Kiswahili miongoni mwa wakazi wa Kampala lakini ni wenyewe wanaorudisha juhudi zao nyuma tena.

Kulingana na mhojiwa mmoja miundo isiyofaa katika lugha ya Kiswahili ni athari kutoka kwa wanahabari. Kuna miundo ya sentensi kama vile,

*Mtoto mwenye ameenda shuleni ni mgonjwa.*

Muundo wa sentensi hii si sahihi kwa sababu kivumishi –enye hakifuatwi na kitenzi. Badala yake, sentensi hii inastahili kuwa: Mtoto aliyeenda shuleni ni mgonjwa.

Kamati ya Mwesigye (2016) ilibaini kuwa Shirika la Utangazaji la Uganda halikuwa linafuata kanuni za kuwaajiri wafanyakazi wake. Wengi wa wafanya kazi hawakuwa na utaalamu na ujuzi tosha wa kufanya kazi walizopewa wakiwemo watangazaji na wahariri wa Kiswahili katika Shirika hili. Upendeleo ulitumiwa sana wakati wa kuajiri na hivyo basi kuathiri shughuli nzima ya kuendeleza na kukikuza Kiswahili jijini Kampala.

**Wataalamu Wachache katika Lugha ya Kiswahili**

Lugha ya Kiswahili imekumbwa na changamoto katika sekta ya utaalam katika Shirika la Utangazaji Uganda. Jambo hili limeathiri juhudi zake za kuendeleza na kukuza lugha ya Kiswahili katika mji wa Kampala. Wataalam waliopo ni wachache na wenye umilisi mdogo katika matumizi ya lugha ya Kiswahili. Hali hii inalingana na maoni ya Odawo na Onyango (2014) walipobaini kuwa waandishi na watangazaji wa habari nchini Kenya hudhihirisha umilisi finyu katika matumizi ya lugha ya Kiswahili. Hali hii husababisha wao kufanya makosa mengi wanapotangaza na kuandika habari katika lugha ya Kiswahili. Hali hii imesababisha wanahabari wengi katika Shirika la Utangazaji Uganda kuwaalika wataalamu kutoka nje ya nchi ya Uganda kufanya mawasilisho ya kuwafunza waandishi na watangazaji wa habari. Kama shirika la habari, Shirika la Utangazaji Uganda halijatoa makala katika lugha ya Kiswahili ili kuwafunza wakaaji wa mji mkuu wa Kampala lugha ya Kiswahili. Jambo hili linatokana na uchache wa wataalam wa kutoa makala haya.

Watafiti chipukizi katika lugha ya Kiswahili kwa hivyo hufa moyo kwa kukosa marejeleo ya kufanya utafiti wao. Wao hupata wakati mgumu kwa sababu wanastahili kutafsiri makala kutoka lugha ya Kiingereza hadi lugha ya Kiswahili. Uchache wa makala pia umesababishwa na uchache wa waandishi katika Shirika la Utangazaji la Uganda. Hii ni kwa sababu ya ufadhili mdogo unaopewa kwa waandishi na watafiti katika lugha ya Kiswahili. Kwa sababu hii, wakaaji wa mji wa Kampala hawapati makala ya kuwafundisha lugha ya Kiswahili. Mhojiwa III alisema:

> ”*Waandishi habari wanaoendeleza shughuli za Kiswahili katika Shirika la Utangazaji la UBC ni wanne, wawili kwa upande wa redio na wawili kwa upande wa TV, ila hakuna aliye na shahada ya umahiri katika Kiswahili miongoni mwa wanne na ni mmoja tu aliye na shahada katika Kiswahili.”*

Shirika la Utangazaji la Uganda lina jukumu la kuikuza lugha ya Kiswahili miongoni mwa wakaaji wa mji wa Kampala. Shirika la Utangazaji la Uganda lina uhaba wa waandishi wa habari, watangazaji wanaoelewa lugha ya Kiswahili pamoja na fani ya uandishi wa habari. Mara nyingi wale wachache ambao wamepatikana huenda wakawa ni walimu au ni watu tu wanaokijua Kiswahili bila ya kuwa waandishi habari au wasomi wa Kiswahili. Wataalam wanaojua Kiswahili bila kujua jinsi ya

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2200

kuwasilisha habari hii kwa lugha ya Kiswahili ni changamoto katika lugha ya Kiswahili kwa sababu ujumbe ufaao huwasilishwa kwa njia isiyofaa. Tatizo hili limefanya Shirika la Utangazaji la Uganda kushindwa kuongezea Kiswahili muda au vipindi ambavyo shirika hili lingeweza kutumia kuendeleza na kudumisha lugha ya Kiswahili miongoni mwa wakaaji wa mji mkuu wa Kampala.

Kwa mfano, uchache wa wataalum katika lugha ya Kiswahili umesababisha lugha ya Kiswahili wakati mwingine kufunzwa katika lugha ya Kiluganda katika Shirika la Utangazaji la Uganda kupitia kipindi cha UBC Star TV maarufu kama *Yiga Oluswayiri*.

**Ukosefu wa Wahisani na Ufadhili**

Tofauti na Kiingereza na Kiluganda, vipindi na habari za Kiswahili ni vigumu nchini Uganda kupata wafadhili ama wasihani. Kwa hiyo jambo hili limepelekea Kiswahili kupewa muda mdogo sana katika Shirika la Utangazaji la Uganda. Kwa mfano, habari za Kiswahili hupewa dakika kumi au kumi na tano katika redio. Hali ni ile ile katika televisheni ambapo habari katika lugha ya Kiswahili hupewa muda wa dakika kumi na tano au thelatini huku Kiingereza na Kiluganda hupewa muda zaidi ya dakika arubaini kwa vile kuna wafadhili. Kwa hiyo kupewa muda mdogo kunabana shirika hilo kuendeleza lugha ya Kiswahili miongoni mwa wakaaji wa mji wa Kampala. Na hata katika kuandaa mashindano ya Kiswahili ya kila mwaka katika Shirika la Utangazaji la Uganda, mashindano hayo hayafani sana kwani wahisani wa lugha ya Kiswahili huwa hawapo ambao wangeweza kutoa zawadi zinazofaa kwa washindi katika lugha ya Kiswahili. Kiingereza na Kiluganda ni lugha ambazo zina wataalamu wengi ambao wanaujuzi wa lugha hizo pamoja na masuala ya uandishi wa habari.

Kwa kukosa wahisani vipindi vya Kiswahili havipewe kipau mbele kwa vile vipaumbele vya shirika hilo ni kuboresha vipindi ambavyo vimewavutia wahisani na wafadhili. Vipindi visivyo na wahisani huwapa wakati mgumu watangazaji wake kwa vile motisha kama viinua mgongo huwa hawapati. Jambo hili huwafanya baadhi ya waandishi habari za Kiswahili wanaojua Kiingereza kuhamia upande wa Kiingereza na kuanzisha vipindi kwa Kiingereza.

**Kutokuwepo kwa Sera Madhubuti ya Uhariri Kuhusu Kiswahili**

Watafitiwa hasa kutoka kwa waandishi wa habari za Kiswahili wanasisitiza kuwa ukosefu wa sera madhubuti kuhusu Kiswahili ndiyo maana maendeleo yake bado yanasuasua. Wanatoa mfano kuwa katika matangazo ya mbashara ya maadhimisho, lugha zinazotakikana kutumiwa ni pamoja na Kiswahili, Kiingereza na Kiluganda, ila tangu Ismail Kigozi astafu mwaka 2018 matangazo ya mbashara kwa Kiswahili wakati wa maadhimisho yamekwama ingawa kuna watu wa kuziba hilo pengo. Kungekuwa na sera madhubuti basi hilo pengo muhimu lingekuwa limezibwa kitambo.

Sera za uhariri huongoza mpangilio na mwelekeo wa vipindi na shughuli katika mashirika ya utangazaji au vyombo vya habari. Sera ya uhariri kuhusu Kiswahili ya Shirika la Utangazaji la Uganda haieleweki ndiyo maana vipindi vya Kiswahili havijaboreshwa na kuimarishwa vyakutosha. Kuwepo kwa kipindi chochote kile cha Kiswahili hutegemea watawala na nia ya mwandishi habari wa Kiswahili wa wakati huo. Ndiyo maana mwandishi habari wa Kiswahili akitoweka basi vipindi au kipindi alichokuwa anafanya pia nacho hutoweka. Mfano Mary Kilobi alipotoka UBCTV na kuhamia Kenya, kipindi chake cha *Tujifunze Kiswahili* kilisimama kwa muda mrefu hadi pale kilipopata mtu wa kukiendeleza. ”Mugisha Shadid alipotoka UBC TV kipindi chake cha *midundo* ya *Kiswahili* nacho kilifutwa.”

**Uhaba wa Vitendea Kazi**

Kamati ya Mwesigye (2016) ilibaini kuwa vitendea kazi ni moja wapo wa changamoto zinazozuia Shirika la Utangazaji la Uganda kutoa huduma za Kiswahili na zilizobora kwa hadhira yake. Kamati hiyo ambayo ilikuwa imeteuliwa

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2200

kuchunguza nafasi na changamoto za shirika la Shirika la Utangazaji la Uganda kwa kuwahudumia wananchi wa Uganda ilisisitiza umuhimu wa Shirika hili kuwa na vitendea kazi bora na vya kutosha. Vitendea kazi kama vinasa sauti, vinasa picha, vifaa vya kuhariri na kuanda filamu, video, na sauti vinavyotumiwa na Shirika hili ni vichache na isitioshe vimepitwa na wakati. Kwa vile vitendea kazi ni vichache, wakati mwingi huhifadhiwa kwa shughuli za Kiingereza na Kiluganda na wala si Kiswahili.

Watafitiwa hasa wale kutoka makao makuu ya Shirika hili walikiri kuwa hata ingawa waandishi habari za Kiswahili wa Shirika la Utangazaji la Uganda wangelipenda kufanya kazi kadri ya uwezo wao, vitendea kazi kutokuwepo hukwamisha juhudi zao hizo. Mashirika kama *British Broadcasting Corporation* na *Deutsch Welle* yameweza kutoa mchango mkubwa wa kuendeleza Kiswahili duniani kwa vile yana vitendea kazi vya kutosha na vya kisasa. Kutokuwepo vitendea kazi huathiri ubora wa habari na vipindi vya Kiswahili, huchelewesha baadhi ya vipindi na makala za redio au televisheni na huwakatisha tama waandishi wa habari.

**Hitimisho**

Makala hii imeonyesha kuwa uhaba wa vitendea kazi, kutokuwepo kwa sera madhubuti ya uhariri kuhusu Kiswahili, ukosefu wa wahisani na ufadhili, wataalamu wachache katika lugha ya Kiswahili, athari kutoka kwa watangazaji, mfumo wa elimu unaoegemea lugha ya Kiingereza na mtazamo hasi kwa lugha ya Kiswahili ni baadhi ya changamoto zinazokumba Shirika la Utangazaji Uganda katika harakati zake za kuendeleza na kukuza lugha ya Kiswahili miongoni mwa Wanauganda hasa wakaaji wa jiji la Kampala.

**MAREJELEO**


Ababaker E. (2013), *Maendeleo ya lugha ya Kiswahili na Athari Zake kwa Jamii ya Kiarabu, Mtazamo wa kilughawiya Jamii.* Tasnifu ya uzamifu katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Victor (2019), *Language Planning in Higher Education*. New York: Oxford University Press.

Kiango J. (2002), Nafasi ya Kiswahili Katika Ujenzi wa Jamii Mpya ya Afrika Mashariki, Swahili *Forum Ix • 143—154*

Miima, F. A. & Kawoya, V. F (2021). Msatakabala na Changamoto za Kiswahili Nchini Uganda. *East African Journal of Swahili Studies, 3(1), 7077.https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.36.*

Haugen, E. (1959), *Planning for a standard language in modern Norway*, Anthropological Linguistics 1(3). 8

King'ei, K, G. . (2000), *Matatizo ya Matumizi ya Lugha Katika Vyombo vya Habari: Mifano Kutoka Kenya, AAP 64: Swahili Forum VII • 45-5*

Haugen na Einar. (1959), *Planning for a standard language in modern Norway, Anthropological Linguistics 1(3). 8*

Mwesigye P. (2016) *Report of the UBC Review Commission, Kampala,* Shirika la Utangazaji la Uganda.

Ryanga na Ngowa (2018) Learning About language: An Introduction to Sociolinguistics. England: Edinburgh Gate.

Mwesigye (2016) Language and power: Longman. Google Scholar

Odawo M. and Onyango J. (2014). Kiswahili kama Chombo cha Kutangaza na Kuuza Vyombo vya Habari nchini Kenya. *MULIKA Journal Number 35, 2016 Pg. 87 97.*

Bamgbose A. (1991), *Language and the nation,* Edinburg. Edinburg, University Press.


 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.